



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE

*Barua zote ziandikwe na kutumwa kwa:*

Tel: +255 262 965732 (Direct line)  
+255 659 566703

e-mail: [ded@sikongedc.go.tz](mailto:ded@sikongedc.go.tz)

Tovuti: [sikongedc.go.tz](http://sikongedc.go.tz)

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)  
Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge  
4 Mtaa wa Bomani  
S.L.P 70

45382 - SIKONGE TABORA

7/06/2023

**TANGAZO**  
**LA**  
**KUTOA HUDUMA YA ULINZI**  
**LGA/121/2023/2024/NC/01**

1. Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge inapenda kuwatangazia wananchi wote wenye Makampuni ya Ulinzi yenye nia na uwezo wa kutoa huduma ya ulinzi katika Ofisi na maeneo mbalimbali yaliyopo ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge. Kazi hii ni kuanzia tarehe 01 Julai, 2023 hadi tarehe 30 Juni, 2024.
2. Unakaribishwa kuleta Kotesheni yako ya bei kwa ajili ya utekelezaji wa kazi kama ilivyoelezwa kwenye Maelezo ya Mahitaji na Bei kama ilivyofafanuliwa katika Sehemu ya II.
3. Vitabu vya Kotesheni vinapatikana katika Ofisi ya Manunuzi na Ugavi Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa bei ya Tsh. 30,000/ kwa Kampuni itakayomba kazi hii
4. Kotesheni zote zitumwe zikiwa zimejazwa nakala halisi (ORIGINAL - MOJA) na (COPY - MBILI) zinazofanana, zilizojazwa kwa usahihi na zilizowekwa kwenye bahasha isiyo na maandishi juu na kuandikwa;

**"KOTESHENI NA. LGA/121/2023 – 2024 /NC/01" KWA UTOAJI WA HUDUMA YA ULINZI KATIKA OFISI NA MAENEO MBALIMBALI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA SIKONGE**

5. Maombi yote yapelekwe (yatumwe) kwa **Katibu wa Bodi ya Zabuni ya Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge, S..L.P 70, SIKONGE.**

6. Mlinzi awe amepitia mafunzo ya Mgambo au JKT na awe mwaminifu kulinda mali za umma
7. Kampuni iwe na uwezo wa kifedha wa kulipa fidia pindi wizi au uharibifu wowote utatokea wakati wa kutekeleza mkataba
8. Kampuni iwe na Leseni halali ya Biashara na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
9. Kampuni ionyeshe utambulisho kwamba inalipa Kodi (TIN Number) na kivuli chake kiambatanishwe kwenye maombi yake
10. Kampuni iwe imesajiliwa na Msajili wa Makampuni na kivuli cha usajili kiambatanishwe kwenye maombi yake
11. Kampuni ionyeshe uzoefu wa Kazi husika
12. Kampuni ionyeshe gharama ya Mlinzi mwenye silaha (**Armed security Guard**) na gharama ya mlinzi asiyekuwa na silaha (**Unarmed security Guard**).
13. Siku ya mwisho ya kuwasilisha Kotesheni ni **siku ya Jumanne tarehe 20.06.2023 saa 5:00 Asubuhi**. Kotesheni zitafunguliwa hadharani mara tu baada ya muda wa mwisho wa kupokea maombi. Ufunguzi utafanyika mbele ya wawakilishi wa wazabuni wanaoamua kuhudhuria katika ufunguaji wa zabuni katika ukumbi mdogo uliopo katika jengo la Idara ya Elimu Sekondari
14. Kotesheni zitakazochelewa, sehemu ya kotesheni, kotesheni za kielektroniki, na kotesheni zisizofunguliwa katika tukio la ufunguaji kotesheni, kwa hali yoyote ile kotesheni hizo hazitakubaliwa kwa tathmini.



Seleman M. Pandawe  
Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**SIKONGE**

**MKURUGENZI MTENDAJI**  
**WILAYA - SIKONGE**